# DAMU IMEMWAGIKA

F.E.M.K. SENKORO

## UTANGULIZI:

Mpiko: Katika kujaribu kumbadili mwanadamu kuna mipaka yake, ambayo mwanadamu yeyote hawezi kuvuka kwa mabadiliko. Huu ndio undani wa mwanadamu.
(Damu Imemwagika - uk. 33)

Ni vizuri kuanzia mjadala kuhusu tamthilia hizi mbili kwa dondoo hilo la Mpiko, mhusika mmojawapo wa tamthilia ya Paulo! Paulo! kwani linagusia suala muhimu lijitokezalo katika tamthilia zote mbili: suala la MABADILIKO. Mabadiliko haya yanatokana na nguvu mbalimbali za kijamii kama vile za kitamaduni, kisiasa na kiuchumi. Na katika nguvu hizo za kijamii mmejificha mivutano na migongano kadhaa. Kati ya hiyo umo ule wa vizazi; na huu hujitokeza katika Paulo! Paulo! na Damu Imemwagika.

Hata hivyo si tamthilia hizi tu ambazo zimelishughulikia suala hili la mgongano baina ya kizazi cha leo (vijana) na cha zamani(wazee). Viko vitabu vingi vya fasihi ya Kiswahili na ya Afrika kwa jumla ambavyo vimeshughulikia masuala yaibushwayo katika tamthilia hizi. Tamthilia za Wakati Ukuta (E. Hussein), Mtawa Mweusi(Ngugi wa Thiong'o) Dilemma of a Ghost(Ama Ata Aidoo), Wala Mbivu (A. Chogo); na riwaya ya Mwenda Kwao(C. Omari) na shairi la Wimbo wa Lawino(Okot p'Bitek) -- yote hii ni mifano ya kazi za fasihi ambazo zimelishughulikia suala la mgongano wa vizazi ambao, kimsingi, ni mgongano baina ya tamaduni zitofautianazo.

Tuuchunguze mgongano huu kwa undani zaidi. Umegawanyika katika sehemu kuu nne:

1. Mgongano uletwao na tamaduni tofauti(huu pia unahusiana na ule kati ya miji na vijiji).

2. Viwango mbalimbali na tofauti tofauti vya elimu.

3. Mfumo wa kiutawala.

4. Matukio ya kihistoria na mabadiliko ya nyakati tofauti.

Tuanze kulichunguza suala hili la mabadiliko lilivyojitokeza kwanza katika tamthilia ya kwanza ya Paulo! Paulo! halafu ndipo tulichunguze katika ile ya Damu Imemwagika.

Katika tamthilia ya Paulo! Paulo! mabadiliko twayaona katika mvutano na mgongano baina ya Paulo na baba yake, Baba-Paulo. Muhtasari wa mgongano na mvutano huu uko katika maneno ya Paulo yalinganishwapo na yale ya Baba Paulo:

Paulo: Hawa wazee wanafikiri dunia yetu ni yao. Hawajui kiendeleacho nchini leo. Wanajua tu nyumbani kwao na kijiji chao na wanasema wameiona dunia kuliko sisi. Kama wameiona dunia kwa kuishi, sisi tumeiona kwa kuisoma. Basi hakuna tofauti.(uk.25)

Katika maneno haya ya Paulo tunagundua mojawapo ya sababu kuu ziletazo utengano baina ya vizazi hivi: ELIMU. Elimu waliyo nayo Paulo na Asifa hadi Chuo Kikuu imewafunza na kuwapa mtazamo tofauti kabisa na wa wazazi wao kuhusu maisha kwa jumla. Paulo anaamini kuwa ana haki ya kujiamulia mambo yake mwenyewe, wakati ambapo baba yake kashikilia mtazamo wa kijadi kuwa mzazi ana madaraka yote juu ya mtoto wake. Amali hizi za jamii ya jadi zinapoasiwa huwafanya akina Baba Paulo wabaki wakilalamika na kuyashangaa yote yatokeayo:

Baba Paulo ..........Tukipanda yeye(Paulo) anashuka Tukisimama yeye anakaa. Kwetu kukiwa jioni kwake ni asubuhi. Lieni jamani dunia yetu imepotea. Tutaulizwa tulikoipeleka...(uk.31).

Kwa maoni ya Baba Paulo, dunia huongozwa na wazee, mabadiliko yote lazima yaelekezwe nao.

Hata hivyo siyo elimu tu ambayo imeleta ufa baina ya vizazi hivi viwili. Mfumo wa kiutawala pia unahusika sana hapa. Sawa na vile ambavyo Tatu na Swai wa tamthilia ya Wakati Ukuta wanavyofunga ndoa kwa Katibu wa Wilaya bila idhini ya wazazi, vile vile Paulo na Asifa wanaoana "Serikalini", bila idhini ya wazazi pia. Mfumo na mabadiliko ya kiutawala kwa jumla yamewanyang'anya wazazi madaraka juu ya watoto wao:

Paulo: Lakini tumeshaoana. Kufuatana na hali ya mambo ya siku hizi yalivyo, serikali inaruhusu kuoana.

Baba Paulo: Serikali, serikali ni nani? Imekuzaa ikuozeshe mke? Ujinga huo utamweleza mama yako. Na nakwambia kwamba tangu sasa utakiondoa hicho kinyongo katika nyumba hii.

Paulo: Yaani__________mbona huelewi? Talaka haiwezekani. Tumeshaoana. Tumekubaliana na imehakikishwa na Mwandishi wa Ndoa huko Dar es Salaam.

Baba Paulo: (Kwa hasira) Mababu wanatuangalia. Je utakiri amri yangu au hapana? (Anamsogelea).

Baba Paulo hatambui umuhimu wa mabadiliko haya, na hajui kuwa lazima yatokee. Hata katika "Utangulizi" twaelezwa na mwandishi kuwa kwa vile mzee huyu "hakuguswa na upepo wa mabadiliko", na kutokana na majivuno yake ndiyo sababu anaanguka. Kwa hiyo swali la nani kamuua Baba Paulo limepatiwa jibu na mwandishi mwenyewe katika "Utangulizi" huo kuwa "Baba Paulo amejinyonga mwenyewe."

Hilo, nionavyo, ni jibu la mkato mno ambalo limelazimishwa na mwandishi kukidhi haja za vigezo mbalimbali vya Tanzia za Kigiriki. Lakini ni dhahiri kuwa nguvu mbalimbali zilizoko nje ya Baba Paulo ndizo hasa zinazowazaa kina Baba Paulo katika jumuia yoyote - nguvu za kiuchumi, kisiasa na kiutamaduni kwa jumla.

Tunaziona nguvu za kiuchumi zikimuathiri Baba Paulo ambaye yu ategemea kupata maelfu ya pesa kutoka kwa kijana wake. Za kisiasa na kiutawala zinajitokeza katika mwingiliano wa kimadaraka baina ya wazazi na serikali juu ya vijana katika jumuia. Nguvu za kiutamaduni zinaibuka katika mfumo wa elimu ambayo huwatenganisha wazazi na vijana. Nguvu zote hizi zinamkabili na kumshinda Baba Paulo; nazo, hatimaye ndizo zinazomwangamiza.

Kutokana na maoni haya basi, itakuwa vizuri kwa msomaji au mtazamaji wa tamthilia hii kujadili suluhisho la mgogoro na mvutano huo, ambalo limetolewa na mwandishi mwenyewe katika "Utangulizi" anaposema:

> Katika jumuia yoyote kuna kina Baba Paulo;
> ingawaje ndugu wa kundi hili hawajijui.

Labda katika tabia fulani nyingine za maisha wachukue wito wa Tujibadilishe, kabla hawajachelewa mno. Baba Paulo wa Paulo! - Paulo! alichelewa mno.(uk.5)

Je ni kweli kuwa suluhisho ni kuchukua tu wito wa Tujibadilishe?

## MABADILIKO NA MGOGORO MKUU KATIKA TAMTHILIA YA DAMU IMEMWAGIKA.

MTEMI: Ndiyo moto, si mzaha, watoto tumewazaa wenyewe, sasa wamekuwa wakubwa,(kimya) wanatugeuka. Wametuasi. Taabu tumepata, vikwazo tumevivuka, vigingi tumeving'oa na mwishowe tumefaulu. Lakini bado vijana wetu wanatugeuka. Tandala(kwa nguvu) imeanguka...(uk.44).

Hayo ni malalamiko ya Mtemi, mwakilishi wa ujadi katika tamthilia hii. Jadi hii inapambana na nguvu mpya, nguvu za kizazi kipya.

Tofauti iliyopo baina ya mgongano tuukutao katika tamthilia ya Paulo! Paulo na huu wa Damu Imemwagika ni kuwa wa Paulo! Paulo ni hasa wa kitamaduni wakati mgongano mkuu katika Damu Imemwagika umejengeka juu ya masuala ya kisiasa.

Tunaweza kuwagawa wahusika wa Damu Imemwagika katika makundi makuu mawili yanayokinzana. Upande mmoja wako Mtemi, Mpambi, Padri, Raia wa 1 na wa 2, Mtu wa kwanza na wa pili, na Mpiga Ramli. Upande wa pili wako akina Matuta, Remi na Makula. Hata hivyo si kuwa kila mmoja katika upande mmoja anapigania kitu hicho hicho kimoja. Mtemi anataka kudumisha jadi ya kiutawala, anataka kudumisha utawala wake wa kitemi. Padri anataka kuendeleza utawala wa kikoloni ambao unamtetea na kumlinda yeye na maslahi yake ya Kipadri. Mpambi, kama asemavyo mwenyewe, "ni mtumwa tu, analotaka Bwana wangu nitalitenda, nitalifanya; sina sauti"(uk.53). Raia wa 1 na wa 2 na Mtu wa 1 na wa 2 - - hawa nao ni watetezi wa ki-bendera kufuata upepo wa Mtemi, sawa na Mpiga Ramli ambaye ni "mtegea nafasi au ufa" ili ajipachike. Kwa hiyo kwa muhtasari tunaweza kusema kuwa hapa kuna mvutano baina ya Tawala za kitemi na kikoloni upande mmoja na nguvu za wananchi zinazodai uhuru kutoka kwa Mtemi na Malkia Elizabeth upande wa pili.

Nguvu hizo za upande wa pili ndizo zinazomkabili na kumshinda Mtemi hadi anaamua kujiua. Mtemi, sawa na Baba Paulo katika Paulo! Paulo!, hajiui kwa sababu ya majivuno, bali anauawa na nguvu za kijamii zinazojitokeza katika madai ya vijana kama akina Matuta, Makula na Remi. Kifo cha Mtemi pamoja na wasiwasi alio nao Padri ni ishara za kushindwa kwa tawala hizo za kitemi na kikoloni. Ni ishara ya ushindi wa nguvu mpya ziongozwazo na kizazi kipya cha vijana. Ni ishara ya ushindi wa madai ya uhuru ya wananchi wa Milesia. Ni ishara ya ushindi wa haki na wema juu ya dhuluma na ubaya.

Dhamira zinginezo

Ziko dhamira zinginezo ambazo zinajitokeza katika tamthilia hizi mbili.

Moja ya dhamira hizo ni ile ihusuyo nafasi ya mwanamke katika jamii. Nafasi hiyo imeonyeshwa kuwa duni mno. Katika Paulo! Paulo!, kwa mfano, tunaigundua nafasi hiyo katika maneno ya Baba Paulo (uk.7):

Baba Paulo: ... Akili yako sawa sawa na ya mama yako. Wanawake siku zote ni viumbe duni tu.

Kazia: Bwana wangu - unafikiri akili ya mwanamke inajaa hapa(Akionyesha kiganja cha mkono). Haijai nakwambia.

Hata hivyo hii haimaanishi kuwa mwanamke yuko kimya tu, kwani katika tamthilia ya Damu Imemwagika tamko la Mama-Remi(uk.56) la "Uchungu wa uzazi tunajua sisi wanawake" ni dalili ya kujizatiti na kutambua umuhimu wa mwanamke si katika kuihudumia tu jamaa bali hasa katika kuendeleza uhai wa jamaa na wingi wake.

Dhamira ya umuhimu wa umoja inajitokeza katika tamthilia ya Damu Imemwagika. Humu, katika ukurasa wa 39 Matuta anasema:

Matuta: Ni kweli hatuna bunduki wala bombom; lakini tunaweza kutumia silaha nyingine: Umoja. Wote tukisimama wima kwa kauli moja kudai haki yetu tutapata.

Pamoja na umuhimu wa umoja huo, pia dhamira ya ukombozi inajitokeza. Sawa na vile ijitokezayo katika tamthilia ya

E.N. Hussein ya Kinjeketile, dhamira hii ya ukombozi inatoa ujumbe kuwa kutetea nchi si dhambi, kama asemavyo Matuta(uk.39).

Matuta: Mzungu alipokuja aliwahamisha wananchi, aliwaondoa kwenye ardhi ili akae yeye... Sasa ndugu zangu, mkoloni kaambiwa, "Tupishe wenye nchi - wewe rudi kwenu Ulaya." Alikataa kuondoka. Je, mtu wa namna hiyo wewe utamfanya nini? Je mtu kupigania nchi yake ni dhambi?

Watu: Hapana! Hapana!
Haki basi, haina budi kutetewa, nayo haki daima hushinda hatimaye.

Dhamira ya nafasi ya watu au viongozi wa dini katika jamii inaibuka katika Damu Imemwagika. Hii twaiona kupitia kwa mhusika mmoja, Padri. Masanja si mwandishi wa kwanza Afrika kuonyesha vile wakoloni walivyowatumia watu wa dini kuilainisha mioyo ya wananchi ili ukoloni uzidi kuwagandamiza. Waandishi wengine maarufu, kwa mfano Chinua Achebe wa Nigeria katika kitabu chake cha Shujaa Okonkwo, Ngugi wa Thiong'o wa Kenya katika vitabu vyake karibu vyote hasa vya A Grain of Wheat, Mtawa Mweusi na Petals of Blood ni mifano ya waandishi ambao wameonyesha vile ambavyo dini huwa ni sehemu tu ya utawala, na kuwa hutetea maslahi ya tawala zozote zinazowapa wakuu wake maslahi yao.

Dhamira ya uongozi bora hali kadhalika inaibuka humu. Wakati ambapo katika Damu Imemwagika dhamira hii inaonyeshwa ikitekelezwa kivitendo na akina Matuta, Makula na Remi, katika Paulo! Paulo! twaona ikilalamikiwa na Mama Paulo(uk.16).

PAULO: Ni mambo kama haya yafanyayo maisha yetu kuwa mafupi... Kila siku serikali inatuhimiza tuwe safi, tule chakula safi, na tufue nguo zetu na mambo kama hayo.

MAMA PAULO: Hao wanasema tu. Tumewaona wapi? Watupe basi vitu hivyo.

PAULO: Siyo hivyo. Sisi wenyewe tunatakiwa tufanye juhudi hata tuiendeleze hali yetu ya maisha.

MAMA PAULO: Na wao wasemao hatuwaoni - tukishampa zawadi kama yai au kuku basi.

Katika malalamiko haya ya Mama Paulo tunagundua ufa uliopo baina ya viongozi na waongozwao, ufa ambao si mara ya kwanza kuonyeshwa katika fasihi ya Kiswahili.

Muhtasari kuhusu Fani katika Tamthilia hizi mbili:

Fani katika tamthilia hizi ni ya moja kwa moja ielewekayo bila matatizo yoyote.

Wahusika kama tulivyokwishaona, wamegawanyika katika makundi makuu mawili. Upande mmoja wako akina Baba Paulo na Mtemi ambao ni "Wanajadi" wakumbwao na mabadiliko wasiyo na uwezo wa kuyazima. Upande wa pili ni wa akina Paulo, Matuta, Makula na Remi wawakilishao nguvu mpya za kitamaduni na kisiasa kwa jumla. Wengi wa wahusika wa kike wamewekwa na waandishi kuwakilisha nafasi duni ya mwanamke katika jamii. Hawa ni akina Mama Paulo, Mama Remi na hata Asifa ambaye ijapokuwa yuko upande mmoja na Paulo, maamuzi yatolewapo kuhusu ndoa yao yu kimya sawa na Mama Paulo na Salia.

Lugha humu ni ya kawaida, na hapa na pale zimetumika nahau, methali na ishara. Kwa mfano uk. wa 15 ipo methali ya "Ukimkumbuka chui funga mlango." Uma na kisu(uk.15) vimetumiwa humu kama ishara za usasa.

Kisanaa, hasa upande wa maonyesho na mpangilio na mtiririko wake, tamthilia hizi zinatofautiana, kwani wakati ambapo maonyesho katika Damu Imemwagika hayana dosari, yale ya Paulo! Paulo! yamekuwa mengi mno kiasi ambacho huenda katika kuigizika kwa tamthilia hii kukawa na matatizo yatokanayo na wingi huo.

Kuhusu kuaminika ama kutokuaminika kwa tamthilia hizi, kwa jumla zote zinaaminika kwani wahusika wake ni watu tuwezao kukutana nao katika maisha ya kawaida, na matukio yake ni ya kawaida yawezayo kutokea maishani.